

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

MKOA WA MARA:
Simu Na.028 2621055
Nukushi .Na.0282621264
Barua pepe: ded@bundadc.go.tz
Tovuti www.bundadc.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:
Kumb Na.HB/W:20/22 VOL:IV/384



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 126,
BUNDA.

01/03/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/377/01/"B"/38 cha tarehe 21/01/2021 cha kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kwa kuzingatia vigezo na maelekezo yaliyopo katika tangazo hili.

1. MTENDAJI WA KIJINI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III) NAFASI 02.

(a) Sifa.

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha IV au VI na awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti cha Technician Certificate (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo - Dodoma au chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

(b) Kazi za kufanya / Majukumu

- Atakuwa Mtendaji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo.
- Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.

- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Atapaswa kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango na maendeleo ya Kijiji.
- Atatafsiri sera, utaratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo za Halmashauri ya Kijiji.
- Atakuwa Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.
- Ataongoza vikao vya maendeleo ya Kijiji vitakavyowahusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umaskini katika eneo lake.
- Atakuwa kiongozi wa Wakuu wa Idara na Vitengo wa kitaalam katika Kijiji.
- Atatekeleza majukumu yote kadri atakavyo kuwa anaelekezwa na mwajiri.

(c) Ngazi ya Mshahara

- Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara Serikalini yaani TGS B1 (390,000/=) kwa mwezi.

(d) Masharti kwa ujumla


- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyewe umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya Kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya taaluma (Professional Certificate from respective board, computer certificate) na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testimonials, Provisional results, Statement of results, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (form IV) na Kidato cha Sita (form VI) **havitakubalika kabisa**.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuhidhinishwa na mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatanishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa, waliofukuzwa kazi na kuachishwa kazi katika utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba

isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

- Barua ya maombi iandikwe **kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili tofauti na hapo ombi lako halitapokelewa.**
- Kichwa cha barua kitaje nafasi ya Kada unayoomba kwa ufasaha.
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi hayo **yatakataliwa.**
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Mwombaji aandike juu ya bahasha nafasi ya kada anayoomba.
- Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usahili kwa kupitia namba za simu na anuani walizotumia kwenye barua ya maombi ya kazi.
- Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 14/03/2021 saa 9:30 Alasiri.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kupitia anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 126,
BUNDA.

Imetolewa na;



Kusaja Amos, J
Mkurugenzi Mtendaji (W)\\
BUNDA

URUGENZI MTENDAJI
MASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

Nakala:- Tangazo ili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na kwenye tovuti (website) ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo ni www.bundadc.go.tz